

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MKUU WA MKOA WA IRINGA



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P 858,
IRINGA.
23/09/2022.

**TANGAZO LA KUTAFUTA MAFUNDI (LOCAL FUND) KWA AJILI YA
KAZI YA UJENZI WA SERVANT QUARTER NA LANDSCAPING KATIKA
NYUMBA YA MAKAZI YA KATIBU TAWALA MKOA.**

Kazi Na. RAS/003/2022-2023/W/01

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa imepokea fedha kutoka Serikali kuu kwa ajili ya Ujenzi wa Servant Quorter na Landscaping katika nyumba ya kuishi Katibu Tawala Mkoa. Ujenzi huo utatekelezwa kwa kuwatumia mafundi kwa utaratibu wa "Force account". Hivyo, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Iringa inawatangazia Vikundi na Mafundi wenyе sifa kwa ajili ya kuomba kufanya kazi tajwa hapo juu.

Maombi yanakaribishwa kwa kikundi au Fundi mwenye sifa zifuatazo:-

1. Mafundi watakaoomba wanatakiwa wawe na uzoefu wakazi za ujenzi zinazofanana na kazi zilizooneshwa. Fundi/kikundi kitatakiwa kuonesha uzoefu/ujuzi wakazi za ujenzi wa majengo makubwa hususani katika taasisi za serikali au watu binafsi. Aidha, waombaji watatakiwa kuambatisha nyaraka zifuatazo; akaunti ya benki anayotumia na kujaza "Vender form" mikataba/barua za taasisi au mwajiri alikowahi kufanya kazi isiyopungua miaka miwili (2) ya hivi karibuni tokea tangazo hili lilinapotangazwa. Aidha, Mwombaji ahakikishe anajaza fomu zilizo katika kabrasha kwa ukamilifu.
2. Tangazo hili linatolewa kwa muda wa siku saba (07) tangu tarehe 23/09/2022 hadi tarehe 29/09/2022.
3. Mafundi wenyе sifa watakaoomba kazi hii wakiwa kwenye vikundi watapewa kipaumbele zaidi.
4. Waombaji wanatakiwa kuwa na mtaji kwa ajili ya kuanzia kazi kwa kulipa vibarua. Malipo yatatolewa na mwajiri kwa awamu baada kazi kufanyika na kukaguliwa na wataalam, ili kuthibitisha ubora na kiwango cha kazi iliyofanyika.

5. Mwombaji lazima aambatishe muda na gharama (labour charge) za kazi aliyoomba na aweke mpango kazi.
 6. Mwombaji awasilishe nakala ya kitambulisho cha mpiga kura/kitambulisho cha taifa/leseni ya udereva, kitambulisho cha Ujasiliamali na TIN namba.
7. Kazi zitakazofanyika ni kama ifuatavyo:-
- i. Kufanya kazi za awali (Preliminaries)
 - ii. Kujenga Msingi wa Jengo (Sub Structure).
 - iii. Kunyanya Jengo (Super Structure).
 - iv. Kuezeka (Roof Structure and covering).
 - v. Kazi ya kuweka milango na Madirisha.
 - vi. Umaliziaji (finishing) wa Jengo.
 - vii. Rangi na mapambo (Painting and decoration).
 - viii. Mfumo wa Maji Safi na taka (Water Supply and Sewage System).
8. Vifaa vyote vya ujenzi (Building Materials) vitatolewa na Mwajiri. Fundi atalipwa gharama ya kazi tu (Labour Charge).
 9. Fundi awasilishe uthibitisho wa kutokuwa ametenda kosa la kijinai, kuwa na mgogoro na serikali
 10. Fundi atatakiwa kuonesha uthibitisho wa kuwa na vitendea kazi muhimu vitakavyomwezesha kukamilisha kazi husika (Mfano:- Pima maji, Mwiko, Birigi (Plumb bob), Water level, Nyundo ndogo za mawe, Chepe (Spade), Kamba manila za kunyoshea na kusetia na vinginevyo.
 11. Nyaraka zinazoonesha michoro, ramani za majengo pamoja na fomu mbalimbali zinapatikana katika Ofisi ya Ununuzi na Ugavi (PMU), OFISI YA MKUU WA MKOA IRINGA, S.L.P 858, IRINGA, kwa gharama ya **Tzs 50,000.00** kuanzia tarehe 23/09/2022 hadi tarehe 29/09/2022, katika Muda wa saa za kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri, Jumatatu hadi Ijumaa.
 12. Maombi ya kazi ya ufundi yaandikwe kwa herufi kubwa yakionesha aina ya kazi uliyoomba, Jina la fundi au Kikundi yawekwe kwenye bahasha isiyo na mchoro wala alama yoyote na yafungwe kwa lakili. Aidha, bahasha ifungwe vizuri. Juu ya bahasha iandikwe jina la kazi uliyoomba. Namba ya kazi husika na anuani ya (KATIBU WA BODI YA ZABUNI, UJENZI WA SERVANT QUARTER NA LANDSCAPING, OFISI YA MKUU WA MKOA IRINGA, S.L.P 858, IRINGA)

13. Maombi yote katika andiko **Halisi moja (1)** na **Nakala (copy) mbili (2)** yaletwe kwenye Ofisi ya Ununuzi na Ugavi (PMU), OFISI YA MKUU WA MKOA IRINGA, S.L.P 858, IRINGA iliyopo katika Jengo la MKUU WA MKOA IRINGA. Muda wa kazi kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.
14. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi hayo ni tarehe 29/09/2022, saa 4.00 asubuhi na maombi hayo yatafunguliwa hadharani mara tu, baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha.
15. Maombi yote ya kazi za ufundi yatakayowasilishwa baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha hayatapokelewa.
16. Siku ya kutembelea eneo la mradi ili kuwezesha kujaza makabrasha itakuwa tarehe 27/09/2022 (Jumanne). Waombaji wote wafike saa 3.00 kamili asubuhi katika jengo la **OFISI YA MKUU WA MKOA IRINGA** ili kuona eneo ulipo mradi kuanzia saa 3.00 kamili asubuhi. Gharama za kutembelea eneo la mradi kila mwombaji atajitegemea.
17. Waombaji wote wanaombwa kuhudhuria katika ufunguzi wa kazi hii katika ukumbi wa Mikutano wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa.



.....
D.M Yinza

**KAIMU KATIBU TAWALA MKOA
OFISI YA MKUU WA MKOA WA IRINGA**